# Utohozi wa Nomino za Kiswahili katika Kimaswamu

*JLLE*
Vol 17(2) 46-80
© The Publisher
DOI: 10.56279/jlle.v17i2.3

*Faraja Mwendamseke*[*]

**Ikisiri**

*Makutano ya lugha katika jamii ni jambo lisiloepukika kutokana na sababu za kihistoria, kisiasa, kielimu, kidini, kiuchumi na kiutamaduni-jamii. Makutano hayo husababisha ukopaji wa maneno. Kutokana na kuwapo kwa mifumo tofauti ya lugha, michakato ya ukopaji hutofautiana kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Lengo la makala hii lilikuwa kuchunguza michakato ya kifonolojia na kimofolojia inayojitokeza wakati wa utohozi wa nomino. Data zilikusanywa mkoani Njombe, nchini Tanzania, katika Wilaya ya Wanging'ombe kwa mbinu za hojaji, usaili na ushuhudiaji. Data zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli, ambapo mbinu ya uchanganuzi kidhamira ilitumika. Nadharia zilizoongoza uchambuzi wa data ni Nadharia ya Fonolojia Zalishi (NFZ), iliyoasisiwa na Noam Chomsky na Morris Halle (1968), pamoja na Nadharia ya Mofolojia Leksika (NML), ambayo mwasisi wake ni Paul Kiparsky (1982). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa wakati wa utohozi wa nomino hizo, michakato ya kifonolojia (uchopekaji, udondoshaji, ubadilishaji sauti na urefushaji wa irabu) na kimofolojia (uambishaji wa kiambishi awali kitangulizi na kiambishi ngeli) hufanyika kwa kufuata kanuni za Kimaswamu ili ziweze kukubalika katika sarufi ya lugha hiyo. Kila mahali palipotokea mabadiliko ya fonimu, kwa kiasi fulani fonimu za Kiswahili zilichukua nduni bainifu za fonimu za Kimaswamu na kuwa na mazingira bayana ya utokeaji. Kutokana na matokeo haya, makala hii inapendekeza utafiti zaidi ufanyike kuhusiana na viarudhi katika maneno ya Kimaswamu yaliyotoholewa kutoka Kiswahili ili kubaini uasilishaji wake. Pia, utafiti ufanyike katika maneno ya aina nyingine kama vile vitenzi ili kubaini michakato ya utohozi.*

**Maneno Msingi:** *Kimaswamu, utohozi, maneno mkopo, mofolojia, fonolojia*

[*] **Corresponding author:**
Lecturer in Linguistics (Kiswahili Unit) in the Department of Languages and Literature at the Dar es Salaam University College of Education, University of Dar es Salaam. E-mail: fmwendamseke@gmail.com

**Abstract**

*Language contact in society is inevitable due to historical, political, educational, religious, economic and socio-cultural reasons. The contact leads to the borrowing of words. Due to the existence of different language systems, borrowing processes vary from one language to another. The aim of this article was to examine the phonological and morphological processes that emerge during borrowing a noun. Data were collected in Wanging'ombe district of the Njombe region of Tanzania, through questionnaire, interview and observation methods. Qualitative approach was employed for data analysis, whereas thematic method was used. The generative phonological theory, developed by Noam Chomsky and Morris Halle (1968), as well as lexical morphology theory, developed by Paul Kiparsky (1982), guided the data analysis process. The findings of the study show that when borrowing nouns, phonological processes (insertion, deletion, sound change and vowel lengthening) and morphological processes (pre-prefixation and noun class prefixation) take place in accordance with Kimaswamu rules so that they are acceptable in the grammar of the language. Wherever there was a phonemic change, Swahili phonemes somehow took over the distinctive features of the Kimaswamu phonemes and manifest a clear context for their emergence. This article recommends further research into prosodic features of Kimaswamu words loaned from Swahili to identify its adaptation. Also, research should be done in other word types such as verbs to identify borrowing processes.*

**Keywords:** *Kimaswamu, borrowing, loan words, morphology, phonology*

## Utangulizi

Watu jamii mbili au zaidi wanaozungumza lugha tofauti wanapotagusana, kuna uwezekano wa kuingiliana kwa matumizi ya maneno ya lugha zao. Katika mawasiliano yao ya kila siku, wazungumzaji hao hujikuta wanatohoa* maneno na kuyatumia. Miongoni mwa mambo yanayowachochea kutohoa maneno ni ukosefu wa maneno ya kutajia dhana au jambo fulani lililo katika lugha nyingine na maendeleo ya kiteknolojia. Iribemwangi na

* Hickey (2010) anaeleza kuwa utohoaji ni sifa mojawapo ya lugha duniani ambayo hutokana na lugha zinazohusika kukutana katika kipindi fulani cha kihistoria lakini uasili wake hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine.

Mukhwana (2011) wanaeleza kuwa utohoaji wa maneno hutokana na kuibuka kwa dhana mpya katika jamii za kilimwengu zinazotokana na maendeleo na mtagusano wa jamii moja na nyingine. Hivyo, ukuaji wa lugha huchochewa na shughuli za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni pamoja na sayansi na teknolojia, kwa lengo la kukidhi mawasiliano kwa wanajamii husika (taz. Pia Lodhi, 2000; Tumbo-Masabo, 2008; Nassor, 2017). Kwa mantiki hiyo, ukopaji wa maneno katika lugha mbalimbali ni suala ambalo hatuwezi kukwepa kulichunguza kutokana na umuhimu wake katika lugha. Thompson (2001) anasema kuwa maneno mkopo yanapotoholewa katika lugha, mambo mawili huweza kutokea: neno linalokopwa huweza kufanyiwa marekebisho ya kifonolojia na kimofolojia au kubaki bila kufanyiwa mageuzi yoyote. Namna utohoaji wa maneno unavyotokea hutofautiana kati ya lugha moja na nyingine (taz. Haugen, 1950; Aswani, 2001; Crystal, 2008; Haspelmath na Tadmor, 2009; Hickey, 2010; Sote, 2011; Lusekelo, 2018; Ola, 2022).

Wazungumzaji wa lugha wanapotohoa maneno, hufuata utaratibu fulani. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa nomino ndiyo maneno yanayokopwa zaidi kuliko maneno mengine (taz., k.m, Olo, 2022; Stephano, 2023). Jambo hili ndilo lilisukuma utafiti huu ushughulikie nomino. Hata hivyo, wataalamu wanatofautiana kuhusu utaratibu wa kufuata wakati wa kutohoa nomino na kuzitumia katika mfumo wa lugha inayotohoa. Wapo wanaodai kuwa nomino za mkopo zinapoingizwa kwenye mfumo wa lugha inayokopa, huzingatia mfumo wa kiisimu wa lugha pokezi (Karuru 2012; Kayigema na Mutasa 2015; Matiki 2016; Msuya na Mreta 2019). Kwa upande mwingine, wapo wanaodai kuwa nomino zinapokopwa huzingatia mfumo wa kiisimu wa lugha changizi (Peperkamp na Dupoux 2003; LaCharité na Paradis 2005; Zibin 2019; Rwamo na Ntiranyibagira 2020). Tofauti hizi za kimtazamo ziliamsha ari ya kuchunguza jinsi nomino za Kiswahili zilivyotoholewa na kuingizwa katika Kimaswamu.

Kimaswamu ni lahaja mojawapo ya Kibena G63. Chaula (1989) anabainisha kuwa Kibena kina lahaja saba ambazo zimepewa

majina kutokana na mazingira yake ya kijiografia. Lahaja hizo ni Kilupembe kinachozungumzwa maeneo ya Lupembe (upande wa Mashariki wa Njombe); Kimasakati kinachozungumzwa maeneo ya Masakati (upande wa Mashariki wa Njombe); Kiilembula kinachozungumzwa maeneo ya Ilembula (upande wa Kaskazini Mashariki mwa Njombe); Kisori kinachozungumzwa maeneo ya Mtwango (upande wa Kati wa Njombe); Kimaswamu kinachozungumzwa maeneo ya Maswamu (upande wa Kaskazini Magharibi mwa Njombe); Kimavemba kinachozungumzwa maeneo ya Kimavemba (upande wa Kusini mwa Njombe); na Kiulanga kinachozungumzwa Wilaya ya Ulanga katika Mkoa wa Morogoro.

Chaula (1989) anaeleza kwamba, licha ya lahaja hizi kuwa na uhusiano wa karibu, zinatofautiana katika mkazo, toni, baadhi ya maneno na sifa kadhaa za kimofolojia na kifonolojia. Data za utafiti huu zinatokana na lahaja ya Kimaswamu ambayo ipo upande wa Kaskazini-Magharibi mwa Njombe.

Kwa upande wa Kiswahili, inaelezwa kwamba ni lugha inayotumiwa na wazungumzaji wengi wa lahaja mbalimbali za Kibena katika nyanja mbalimbali kama vile elimu, siasa, dini na kadhalika (taz. Morrison, 2011; Chaula, 2017). Kwa mujibu wa Chaula (2017), matumizi haya yamechangia athari kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki katika lahaja mbalimbali za Kibena. Mathalani, Kimaswamu kimetohoa maneno mbalimbali kutoka lugha ya Kiswahili.


Makala hii ilichunguza michakato ya kifonolojia na kimofolojia katika kutohoa nomino. Michakato ya kifonolojia na kimofolojia ni mabadiliko yanayoathiri vipandesauti na mofu ambavyo hufuatana katika kuunda neno. Hivyo, sheria/kanuni zinazoongoza michakato mahususi zimebainishwa, ambapo imewekwa wazi kuwa taratibu za mfumo wa Kimaswamu huzingatiwa kwa kiasi kikubwa wakati wa utohozi. Utafiti huu utasaidia katika ufundishaji wa lugha ya pili kwa sababu vikwazo vya kifonolojia vya lugha hizi mbili vimewekwa bayana.

Kabla hatujaonesha michakato ya kifonolojia na kimofolojia ya maneno ya Kimaswamu yaliyotoholewa kutoka Kiswahili, ni muhimu kuonesha mfumo wa fonimu za Kimaswamu kwa ufupi.

**Fonimu katika Kimaswamu**

Kimaswamu kina irabu tano. Irabu hizi zinabainishwa kwa kuzingatia mahali pa kutamkia, mwinuko wa ulimi na mkao wa midomo. Kielelezo Na. 1 kinaonesha irabu hizo.

**Kielelezo Na 1: Irabu za Kimaswamu**




**Chanzo:** Mwendamseke (2011)

Kielelezo Na 1 kinaonesha kuwa Kimaswamu kina irabu 5 kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu kama vile Kiswahili. Irabu hizo tano zimegawanyika kama ifuatavyo: mbele-juu /i/ nyuma-juu /u/; mbele-kati /ɛ/; nyuma-kati /ɔ/ na chini /a/. Mifano ya maneno yenye irabu hizi inaoneshwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Mifano ya Maneno Yenye Irabu za Kimaswamu**

| Alama za Kifonetiki | Alama za Kiothografia | Mfano | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /a/ | a | amuula | amua |
| /ɛ/ | e | epwaali | yupo |
| /i/ | i | ilibiihi | mti |
| /ɔ/ | o | Umgogoolo | mzee |
| /u/ | u | Uwutiine | unga |

**Konsonanti za Kimaswamu**

Kimaswamu kina sauti za konsonanti 19. Konsonanti hizo katika namna ya utamkaji na mahali pa matamshi zinaoneshwa katika Jedwali Na. 2 hapa chini:

**Jedwali Na. 2: Namna ya Utamkaji na Mahali pa Matamshi – Konsonanti za Kimaswamu**

| Namna ya Utamkaji | | Mahali pa Matamshi | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Midomo | Midomo-meno | Meno | Ufizi | Kaakaagu-mu | Kaakaa laini | Glota |
| Vipasuo | Ghuna | b | | | d | | g | |
| | Sighuna | p | | | t | | k | |
| Nazali | | m | | | n | ɲ | ŋ | |
| Vikwamizi | Ghuna | | v | | | | | |
| | Sighuna | | f | | s | | | h |
| Vizuio–Kwamizi | Ghuna | | | | dz | j | | |
| | Sighuna | | | | | | | |
| Vitambaza | | | | | l | | | |
| Viyeyusho | | w | | | | j | | |

**Chanzo:** Mwendamseke (2011)

Mifano ya maneno yenye konsonanti hizo inaoneshwa katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3: Mifano ya Maneno Yenye Konsonanti za Kimaswamu**

| Alama za Kifonetiki | Alama za Kiothografia | Mfano | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /p/ | p | palubaali | pembeni |
| /b/ | b | baaha | hapa |
| /t/ | t | taniila | tania |
| /d/ | d | idaanda | damu |
| /k/ | k | ilikaang'a | yai |

| Alama za Kifonetiki | Alama za Kiothografia | Mfano | Kiswahili |
|---|---|---|---|
| /g/ | g | igoolo | jana |
| /f/ | f | Fuva | fua |
| /v/ | v | vemba | lia |
| /s/ | s | isagaala | kuni |
| /dz/ | dz | dzaguula | chagua |
| /h/ | h | heudza | ondoa |
| /j/ | j | iijiiho | kijiko |
| /m/ | m | amayaao | viazi |
| /n/ | n | Nofu | nzuri |
| /ɲ/ | ny | nyenye | ninyi |
| /ŋ/ | ng’ | ing’aasi | njia |
| /l/ | l | lamuula | amua |
| /j/ | y | yuula | yule |
| /w/ | w | uwutiine | unga |

**Nadharia Zilizotumika katika Utafiti Huu**

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Fonolojia Zalishi (kuanzia sasa NFZ) iliyoasisiwa na Noam Chomsky na Morris Halle (1968) pamoja na Nadharia ya Mofolojia Leksika (kuanzia sasa NML) ambayo mwasisi wake ni Paul Kiparsky (1982). Nadharia hizi zilikuwa mwafaka katika utafiti huu kwa sababu zinaonesha wazi michakato ya kifonolojia na kimofolojia iliyotumika katika kutohoa nomino. NFZ ilitumika katika kuchanganua michakato ya kifonolojia na NML ilitumika katika kuchanganua michakato ya kimofolojia.

NFZ ina misingi mitatu. Mosi, maumbo na miundo yote ya lugha ya binadamu hutokana na umbo la ndani. Pili, maumbo na miundo ya maneno tutamkayo katika vinywa na kusikika huwakilisha umbo la nje, umbo ambalo kwa kiasi kikubwa huakisi umbo la ndani moja kwa moja au baada ya kufanyiwa marekebisho kidogo. Tatu, sauti zote zitumikazo katika lugha asilia za binadamu hutokana na mifumo ya mikondohewa. Nne, NFZ inasisitiza kuzingatia

mabadiliko yanayotokea sauti zinapokaribiana. Katika kiwango cha kifonolojia, fonimu mbili zinapokutanishwa, kuna mambo mawili yanayoweza kutokea: mabadiliko katika kipandesauti kimojawapo kati ya vile vinavyohusika (au vyote viwili) au kutokuwa na mabadiliko yoyote. Mbali na misingi hiyo, NFZ inafanya kazi kwa kuegemea katika mihimili minne (taz. Massamba 2011; Jensen, 2004). Kwanza, katika uwakilishi wa vipengele vya fonolojia na fonetiki, zitumike nduni bainifu ambazo huzitofautisha sauti zinazohusika. Pili, vipengele vyote vya kifonolojia viwakilishwe katika mstari mmoja (uwakilishi moza) ambapo sifa za kiarudhi huchukuliwa kuwa ni vijenzi vya sauti inayohusishwa na sifa hizo. Tatu, kuwepo kwa sheria na kanuni zilizo rasmi na madhubuti zinazoweza kutumika kulikokotoa umbo la nje kutoka umbo la ndani. Nne, kuwapo kwa mpangilio rasmi, madhubuti na usio badilifu wa jinsi ya kuzitumia sheria na kanuni katika kulikokotoa umbo la nje kutoka umbo la ndani. Tano, kuwapo na sababu kuntu zinazoelezea kwa nini uchanganuzi fulani wa data ndio unaonekana kuwa bora zaidi kuliko uchanganuzi mwingine kuhusu data hiyohiyo.

Misingi na mihimili ya nadharia hii ilituongoza katika kuonesha mazingira maalumu ya uzalishaji wa nomino mkopo katika Kimaswamu. Imebainika kuwa kila mchakato una sheria/kanuni zinazoongoza uzalishaji wa nomino hizo katika Kimashamu. Pia, sheria hizo hutawaliwa na nduni bainifu zinazosababisha mabadiliko yatokee kulingana na mfumo wa kiisimu wa Kimaswamu. Hivyo, nadharia hii ilituongoza katika kuchanganua michakato ya kifonolojia inayojitokeza katika kutohoa nomino za Kimaswamu na kuunda kanuni za michakato hiyo.

Utafiti huu umetumia pia NML kama ilivyoelezewa hapo awali. Kihistoria, NML ni nadharia iliyoasisiwa miaka ya 1980 kwa minajili ya kushughulikia masuala ya maumbo ya maneno katika lugha. Hivyo, nadharia hii imekuwa ikitumika kwa muda mrefu kujadili na kufafanua michakato mbalimbali ya kiisimu katika lugha. Kulingana na NML, maneno yanapotoholewa kutoka lugha changizi, huingia katika lugha pokezi kwa kufuata kanuni za

kimofolojia. Aidha, NML inadai kuwa, katika kufuata kanuni hizo, michakato mbalimbali hutumika, hasa kwa minajili ya kuyafanya maneno yanayotoholewa kutoka lugha changizi yakubalike katika lugha pokezi.

NML inazingatia dhana ya viwango vya uchanganuzi. Huona kuwa michakato ya uambikaji huweza kupangwa katika mfululizo wa viwango. Kila kiwango kinahusishwa na seti ya sheria za kifonolojia na ndicho huamua mawanda ya utamkaji wa neno husika. Upangiliaji wa viwango hivi pia ndio huamua upangiliaji wa michakato ya kimofolojia katika kuunda maneno.

Katika mkabala huu, inachukuliwa kuwa umbotokeo la kila uundaji wa maneno, katika leksika, huingizwa katika sheria. Kiparsky (1982) anaeleza kwamba sheria za fonolojia ya leksika hufanya kazi kimzunguko katika lugha, yaani hufanya kazi kwa kurudiarudia baada ya kila hatua katika kila kiwango cha mofolojia. Aina hii ya unyambulishi kimpangilio hujulikana kama mzunguko na hatua/ngazi mahsusi katika mchakato huo ndizo huitwa kiwango. Kanuni zinazojirudia katika kila kiwango huitwa kanuni za kimzunguko (Rubach, 1984).

Kwa kutumia nadharia hiyo, leksika huundwa kwa utaratibu ufuatao: Mofolojia ya kiwango cha kwanza inaingizwa kwenye sheria za kifonolojia za kiwango cha kwanza. Umbotokeo lake linakuwa ni mofolojia ya kiwango cha pili. Mofolojia ya kiwango cha pili huingizwa kwenye sheria za kifonolojia za kiwango cha pili. Umbotokeo lake ni mofolojia ya kiwango cha tatu, ambalo nalo huingizwa kwenye sheria za kifonolojia za kiwango cha tatu. Hali hii huendelea kuwa hivyohivyo hadi hapo viwango vya mofolojia vinapokwisha.

Katika utafiti huu, NML imetuonesha hatua kwa hatua michakato ya kimofolojia iliyotumika wakati wa kutohoa nomino za Kimaswamu kutoka katika Kiswahili. Kwa mantiki hiyo, nadharia hii ilikuwa mwafaka katika utafiti huu kwani ilituongoza katika kuchunguza na kuchanganua mabadiliko ya maumbo yanayojitokeza baada ya nomino zilizotoholewa kutoka katika Kiswahili na kuingizwa

katika Kimaswamu kwa kuwekewa viambishi awali vitangulizi na viambishi ngeli. Pia, nadharia hii imeonesha kwa uwazi sheria za kupachika viambishi hivyo katika nomino za Kimaswamu zilizotoholewa kutoka Kiswahili.

## Methodolojia

Utafiti huu ulitumia data za msingi kutoka uwandani, mkoani Njombe, nchini Tanzania. Data zilikusanywa kutoka katika vijiji vya Imalinyi na Ikangamwani katika Wilaya ya Wanging'ombe. Watoataarifa walipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa na usampulishaji nasibu tabakishi. Katika mbinu ya usampulishaji lengwa, mtafiti alijielekeza kwa wazungumzaji wazawa wa Kimaswamu, ila wazungumzaji hawa walikuwa wanazungumza Kiswahili pia. Baada ya hapo, mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ilitumika kuwapata watoataarifa wachache kutoka kwenye kundi kubwa. Idadi ya watoataarifa waliohusishwa ni 20. Kwa jumla, data iliyotumiwa ilikuwa ya maneno 250 na yalitosha kushughulikia utafiti huu. Data hii ilikusanywa kwa mbinu za hojaji, usaili na ushuhudiaji.

Dawson (2002) na Kothari (2004) wanasema kuwa ni vizuri kutumia mbinu mbalimbali ili kumsaidia mtafiti kukusanya taarifa zote muhimu na za ziada kutoka kwa watoataarifa na mazingira yao kwa jumla. Katika njia ya hojaji na usaili, watoataarifa waliombwa wataje dhana ngeni kama vile aina ya mavazi, huduma za jamii, mavazi, vifaa vya teknolojia, zilizoingia katika utamaduni wao na maneno wanayotumia kuzitaja. Ikumbukwe tumeshaeleza tulitumia watoatarifa 40 katika utafiti huu. Katika hojaji, watoataarifa 8 wanaojua kuandika walihusika. Usaili ulihusisha watoa taarifa 12. Katika usaili, idadi ya watoataarifa ilikuwa kubwa kuliko katika mbinu ya hojaji kwa sababu njia hii ilisaidia kupata data kwa kina zaidi kwa kuwa ilimwezesha mtafiti kuuliza maswali zaidi pale alipohitaji ufafanuzi zaidi. Aidha, mbinu ya ushuhudiaji ilitumika katika kusikiliza masimulizi mbalimbali kutoka kwa wazungumzaji wazawa wa Kimaswamu. Mtafiti aliwaomba watoataarifa 5 kati ya waliofanyiwa usaili wasimulie masimulizi mbalimbali kama vile kuhusu kilimo, mavazi, dini, teknolojia na vyakula. Kila mmoja

alisimulia jambo moja. Zoezi hili liliambatana na kudondoa nomino za mkopo katika mazungumzo yao. Ushuhudiaji uliotumika katika utafiti huu ni ushuhudiaji funge. Njia hii ya ushuhudiaji ilimpa mtafiti uhuru wa kuchanganya na njia ya usaili; na hivyo, kupata nomino mbalimbali zilizotoholewa na kubaini namna ya kutokea kwake.

Katika usaili na ushuhudiaji, data zilirekodiwa kwa kutumia simu ya mkononi kwa ridhaa ya watoataarifa. Baada ya kukusanya data hizo, nomino zilizohusika ziliorodheshwa kwa kuzingatia viambishi kabla ya viambishi awali na yalinukuliwa kwa kuzingatia taarifa za kifonetiki; yaani, nduni bainifu ziliwekwa bayana. Katika uchanganuzi wetu, tulitumia kanuni za NFZ katika kuainisha sauti. Kufanya hivyo kulitusaidia kutambua sauti zilizobadilika. Sheria na vigezo vya kifonolojia vilivyotumika viliwekwa wazi baada ya kuchunguza mabadiliko ya sauti. Pia, tulitumia kanuni za NML katika upachikaji wa viambishi awali tangulizi na viambishi ngeli. Kanuni za fonolojia na mofolojia ya Kimaswamu ndizo zilizoelezea mabadiliko ya maneno.

Aidha, utafiti huu ulitumia mkabala wa kitaamuli katika kuwasilisha na kuchanganua data, ambapo mbinu ya uchanganuzi wa kidhamira ilitumika. Mbinu hii inahusisha mawazo ya jambo linalochunguzwa kwa kuangalia namna linavyojitokeza katika data zilizokusanywa. Maelezo na michoro vilitumiwa kuwasilisha matokeo ya uchunguzi wetu. Maelezo yalitusaidia katika ufafanuzi wa fonimu na mofu. Ufafanuzi zaidi wa vigezo vya kifonetiki ulifanywa kwa kutumia alama husika kama Kiambatisho Na. 1 kinavyoonesha.

## Utohozi katika Kimaswamu

Utafiti huu umebaini kuwa utohozi wa nomino za Kiswahili katika Kimaswamu una athari za kifonolojia na kimofolojia. Aidha, utohozi huo unafanyika kwa kutokea kwa michakato kadhaa ya kifonolojia na kimofolojia. Michakato hiyo hujitokeza wakati wa kuasilisha nomino ngeni katika Kimaswamu. Ikumbukwe kuwa tofauti za kifonolojia na kimofolojia miongoni mwa lugha hupelekea kuwe na tofauti fulani wakati wa kuasilisha maneno yaliyotoholewa

kutoka lugha changizi ili yaendane na mfumo wa lugha pokezi. Ili kubainisha hili kwa uwazi, sehemu hii inaelezea michakato ya kifonolojia na kimofolojia kwa kutumia nomino mkopo zilizotajwa na watoataarifa uwandani. Kwanza, michakato ya kifonolojia ndiyo inaanza kuelezwa kisha inafuata michakato ya kimofolojia.

## Michakato ya Kifonolojia

Michakato ya kifonolojia hutokea katika mazingira tofautitofauti ya neno. Michakato hiyo husababisha mabadiliko katika vipandesauti vimojawapo kati ya vile vinavyohusika katika neno. NFZ imetumika kuonesha mabadiliko haya katika muundo wa nomino kwa kutumia sifa msingi za fonimu husika, yaani kuwepo (+) au kutokuwepo kwa sifa (-) fulani. Michakato ya kifonolojia katika utohozi wa nomino za Kimaswamu inajitokeza kama inavyoelezwa katika aya zinazofuata.

### Uchopekaji

Uchopekaji huhusu kuingiza kipashio ambacho hakikuwepo awali katika mazingira maalum ya kifonetiki. Kwa mujibu wa data zilizokusanywa, kuna uchopekaji wa namna mbalimbali katika Kimaswamu. Mosi, katika Kimaswamu, kuna uchopekaji wa irabu ambao hufanyika ili kuifanya nomino iliyokopwa ifuate utaratibu wa msamiati wa Kimaswamu. Mchakato huo unajidhihirisha katika baadhi ya nomino za Kimaswamu, kama Data Na. 1(a-e) inavyoonesha kwenye nomino zinazohusika. Mchakato huu unajitokeza kwa kiasi kikubwa katika nomino nyingi zilizotoholewa katika Kimaswamu kutoka Kiswahili.

Data Na. 1

*a.* *umukiliisiti*
*u-mu-kiliisiti*
*kat*-1**-kiliisiti*
"Mkristo"

*b.* *umufalaansa*
*u-mu-falaansa*
*kat-1-falaansa*
"Mfaransa"

---

* Kiambishi awali tangulizi; sehemu zote tulipotumia kifupisho hicho tunarejelea hivyo.
** Namba hii inarejelea ngeli ya kwanza; sehemu zote tulipotumia namba 1, 2, 3 na kadhalika ndani ya data tunarejelea ni ngeli ya ngapi.

c. *ikiliiniki*
*i-Ø*-kiliiniki*
*kat-9-kiliiniki*
"kliniki"

d. *ipulasiitiki*
*i-Ø-pulasiitiki*
*kat-9-pulasiitiki*
"plastiki"

e. *iliteleekita*
*i-li-teleekita*
*kat-5-teleekita*
"trekta"

Data Na. 1(a-e) inaonesha nomino za Kimaswamu zilizotoholewa kutoka Kiswahili kwa kuchopekwa irabu mbalimbali. Lengo ni kuyafanya yawe na muundo wa silabi wa KI unaokubalika katika Kimaswamu, kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu, yaani, kwa kawaida, ni lazima silabi iishie na irabu. Ruwaza hii inazuia silabi kuishia na konsonanti pekee. Kutokana na ruwaza ya data tuliyoitumia tunaunda kanuni ya jumla ifuatayo kwa kutumia sifa bainifu za kimatamshi:

Ø > + Sila / +Kons__ +Kons

Kanuni hii inaeleza kuwa irabu ambayo haikuwepo huchopekwa kupata muundo wa silabi kubalifu katika mazingira ya kuwa kati ya konsonanti na konsonanti. Msingi mmojawapo wa NFZ unaeleza kuwa maumbo na miundo yote ya lugha hutokana na umbo la ndani ambalo hujengeka akilini mwa msemaji tangu anapoanza kuamilia lugha mpaka anapopata umilisi kamili wa lugha husika. Hivyo, uchopekaji wa irabu katika Kimaswamu unadhihirisha wazi kuwa kanuni za miundo ya silabi hufanyika kulingana na umilisi alionao mzungumzaji wa Kimaswamu ili kuhakikisha nomino mkopo zinaendana na mfumo wa lugha ya Kimaswamu. Kwa mantiki hiyo, mchakato huu unalenga kuibua muundo wa silabi kubalifu katika Kimaswamu. Hii inadhihirisha umajumui uliopo wa baadhi ya vipengele vya kifonolojia katika lugha za Kibantu. Licha ya umahususi wa lugha, kuna baadhi ya vipengele vinavyofanana. Dhana ya kuwepo kwa mfanano wa baadhi ya

*Kiambishi kapa

vipengele vya kifonolojia kama vile uchopekaji huu imeelezwa pia na Aswani (2001), Sote (2011), Adolph (2014) na Mosota (2016). Hii inadhihirisha kuwa lugha nyingi za Kibantu kama ilivyo katika Kimaswamu haziruhusu mfuatano wa K na K katika neno. Kutokana na mifano tuliyotumia Kimaswamu hakiruhusu mfuatano wa 'm', 'kr', 'kl', 'kt', 'pl', 'tr', 'st' katika muundo wa silabi. Iribemwangi (2010) anasema kuwa, katika Kiswahili, uchopekaji hutumika kwa wingi katika maneno mkopo ya Kiswahili kwa lengo la kuepuka silabi funge mwishoni mwa neno (au silabi) na kuibua muundo wa silabi unaopendelewa na lugha ya Kiswahili wa KI.

Vilevile, katika data za utafiti huu, imebainika kuwa kuna uchopekaji wa konsonanti na kiyeyusho. Katika Kimaswamu, kiyeyusho /w/ na konsonanti /h/ na /l/ huchopekwa katika muundo wa silabi. Data Na. 2(a-e) inadhihirisha mchakato huu wa uchopekaji wa kiyeyusho na konsonanti katika nomino za Kimaswamu.

Data Na. 2

*a.* *ibulawuuzi*
*i- Ø -bulawuuzi*
*ka*t-9-*bulawuuzi*
"blauzi"

b. *itawuusi*
*i- Ø -tawuusi*
*kat-9-tawusi*
"tausi"

*c.* *ifideeho*
*i-fi-deeho*
*kat-8-deeho*
"video"

*d.* *isidiihi*
*i- Ø -*s*idiihi*
*kat-9-sidiihi*
sidii

*e.* *iilaatu*
*i-i-laatu*
*kat-7-laatu*
"kiatu"

Tunaona katika Data Na. 2(a na b) kuwa maneno yaliyotoholewa

yamechopekwa kiyeyusho /w/ ili kutengua milolongo ya irabu iliyopo kwenye maneno ya lugha changizi. Vilevile, katika Data Na. 2(c na d), kuna uchopekaji wa konsonanti /h/ ili kutengua mlolongo wa irabu na kulifanya neno linalotoholewa liweze kutamkwa kirahisi katika Kimaswamu kama ilivyoelezwa hapo awali. Vilevile, Data Na. 2(e) inaonesha uchopekaji wa konsonanti /l/ ambayo pia inatokea katika mazingira ya kuwa kati ya irabu moja na irabu nyingine. Kutokana na ruwaza ya data tuliyoitumia tunaunda kanuni ya jumla ifuatayo kwa kutumia sifa bainifu za kimatamshi:

Ø > + kons/+kiye +irabu__ +irabu

Kanuni hii inaeleza kuwa konsonanti au kiyeyusho ambayo haikuwepo huchopekwa kupata muundo wa silabi kubalifu katika mazingira ya kuwa kati ya irabu na irabu. Aidha, katika data inaonesha irabu zinazofanana huandikwa kwa kufuatana kama vile /ee/, /aa/ na /uu/, hapa ni urefushaji wa irabu na sio mfuatano wa irabu. Uchopekaji wa kiyeyusho /w/ na konsonanti /h/ na /l/ unadhihirishwa na msingi mmojawapo wa NFZ unaoeleza kuwa maumbo ya nje hutamkwa kulingana na mfumo wa lugha inayohusika na mabadiliko yote husabishwa na mazingira fulani kama tuliyoyaeleza katika kanuni. Uchopekaji huu wa konsonanti au kiyeyusho kati ya irabu na irabu unadhirisha hali ya kihistoria katika lugha nyingi za Kibantu kuwa ni nadra sana irabu kufuatana. Ili kuepuka hilo katika utamkaji, lazima kuwe na konsonanti katikati ili kulinda muundo wa silabi (taz. Kang, 2003; Msuya na Mreta, 2019). Hata hivyo, katika Kimaswamu, upekee umejitokeza kwa kuwa na uchopekaji wa kiyeyusho kwa sababu ni jambo ambalo halijitokezi katika lugha baadhi ya lugha nyingine za Kibantu, kama inavyojitokeza katika tafiti za Adolph (2014) lugha ya Kihaya, Mosota (2016) lugha ya Kigusii na Adicka (2016) lugha ya Kijaluo.

## Udondoshaji

Kwa mujibu wa data za utafiti huu, mchakato wa udondoshaji katika Kimaswamu huweza kufanyika mwanzoni mwa nomino. Aidha, katika utafiti huu, imebainika kuwa konsonanti ndiyo inayodondoshwa, kama Data Na. 3(a-c) inavyoonesha.

Data Na. 3

*a.* *iitaabu*
*i*-i-*taabu*
*kat*-7-*taabu*
"kitabu"

*b.* *iikoombe*
*i*-i-koombe
*kat-7-kombe*
"kikombe"

*c.* *iilaatu*
*i*-i-*laatu*
*kat-7-latu*
"kiatu"

Data Na. 3(a-c) inaonesha kuwa sauti /k/ katika nomino zilizokopwa imedondoshwa. Tunaona kuwa sauti /k/ inapokuwa mwanzoni mwa nomino kabla ya irabu, hudondoshwa. Kutokana na ruwaza ya data tuliyoitumia tunaunda kanuni ya jumla ifuatayo:

/k/ → [ø] /-I/ (udondoshaji mwanzoni mwa neno)

+ Kons > Ø __ + Irabu

Kanuni hiyo inaonesha wazi kabisa kuwa udondoshaji huo hutokea pindi konsonanti /k/ inapokuwa mwanzoni mwa neno na kufuatiwa na irabu. Udondoshaji katika Kimaswamu unatokea kwa sababu za kifonolojia za urahisishaji wa matamshi. Nomino hizo zinapatikana katika ngeli ya 7 {hi} katika Kimaswamu. Hivyo, sauti /k/ hurahisishwa na kuwa /h/, ambacho ni kikwamizi hafifu cha koromeo. Hata hivyo, katika mazungumzo, sauti hiyo /h/ hudondoshwa. Hatimaye, sauti hiyo haisikiki, bali kinasikika kilele chake ambacho ni irabu /i/ ya mbele, juu. Haya yanadhihirika katika NFZ ambayo inaeleza kuwa badiliko lolote la fonimu zinazohusiana kiuamilifu utamkaji wake huukiliwa na kanuni zilizo rasmi, wazi na hutokea kihatua katika kuibua muundo wa nje kutoka muundo wa ndani katika mfuatano maalumu. Boen (2014) na Mosota (2016) wanaonesha kuwa udondoshaji kama huo unaweza kutokea ili kuepuka sauti ambazo hazipo katika mfumo wa lugha husika au kutokana na mabadiliko ya kihistoria. Vilevile, udondoshaji katika Kimaswamu upo tofauti na baadhi ya lugha

za Kibantu, kama vile Kimalila. Sote (2011) anaeleza kuwa katika lugha ya Kimalila, upo uwezekano wa silabi yote kudondoshwa katika nomino. Anatoa mifano katika lugha ya Kimalila kama vile *isipitali*, *ikalata* na *imptula*. Katika Kiswahili ilikuwa *hospitali*, *kalatasi* na *kaptula*. Hivyo, silabi $*ho*$ na $*si*$ zimedondoshwa.

## Mabadiliko ya Sauti

Utafiti huu umebaini kwamba katika Kimaswamu, kuna mchakato wa kubadilisha sauti. Hii ina maana kuwa sauti fulani inatumika badala ya sauti nyingine iliyopo katika lugha changizi. Data inaonesha kuwa, katika Kimaswamu, sauti /s/ hutumika badala ya sauti /ʃ/, /ð/ na /q/. Maneno ya Kiswahili yanapotoholewa huwa na mabadiliko kadhaa yanayotokea kwa sababu ya tofauti zilizopo kati ya konsonanti za Kimaswamu na zile za Kiswahili. Kimaswamu hakina konsonati /ʃ/, /ð/ na /q/. Kwa hivyo, lugha hii inapokumbana na sauti hizo ngeni, huzigeuza na kuzifanya zitamkwe sauti ambazo zinafanana kifonetiki na zile za Kimaswamu. Kudhihirika kwa mabadiliko ya sauti hizo kunaoneshwa katika Data Na. 4(a-h).

Data Na. 4

*a.* *isuule*
*i-Ø-suule*
*kat-9-suule*
"shule"

*b.* *isamupeeni*
*i-Ø-samupeeni*
*kat-*9-*samupeeni*
"shampeni"

*c.* *isaambi*
*i-Ø-***s***aambi*
*kat-9-saambi*
"dhambi"

*d.* *isamaana*
*i-Ø-samaana*
*kat-9-***s***amaana*
"dhamana"

*e.* *isumuuni*
*i-Ø-***s***umuuni*
*kat-9-sumuuni*
"thumuni"

f. *isamaani*
*i-Ø-samaani*
*kat-9-**s**amaani*
"thamani"

Data Na. 4(a na b) inaonesha kuwa fonimu /**s**/ ya Kimaswamu imetumika badala ya fonimu /ʃ/ katika nomino hizo zilizotoholewa. Mahusiano baina ya fonimu hizi ni kuwa zote ni vikwamizi. Hivyo basi, /s/ ya Kimaswamu imetumika badala ya fonimu ya Kiswahili /ʃ/ ambayo haipo katika Kimaswamu katika harakati za ukopaji wa nomino. Mabadiliko ya fonimu hizi yanaukiliwa na nduni bainifu zinazohusiana kama ifuatavyo:

| /ʃ/ | → | /s/ |
|---|---|---|
| + konso | | +konso |
| + konti | ⟹ | +konti |
| - ghuna | | - ghuna |
| - ante | | +ante |
| +koro | | +koro |

Hapa tunaona sifa zote zinafanana kasoro sifa ya uanteria ndio inatofautiana katika sauti hizo.

Pia, Data Na. 4(c na d) inaonesha kuwa sauti /s/ hutumika badala ya sauti /ð/. Mahusiano baina ya fonimu hizi ni kuwa zote ni vikwamizi ambavyo. Hivyo basi, fonimu /s/ ya Kimaswamu imetumika badala ya fonimu ya Kiswahili /ð/ ambayo haipo katika Kimaswamu katika harakati za ukopaji wa nomino. Mabadiliko ya fonimu hizi yanaukiliwa na nduni bainifu zinazohusiana kama ifuatavyo:

| / p / | → | /s/ |
|---|---|---|
| + konso | | +konso |
| + konti | ⟹ | +konti |
| + ghuna | | - ghuna |
| + ante | | + ante |

Hapa tunaona sifa zote zinafanana kasoro sifa ya ughuna ndio inatofautiana katika sauti hizo.

Hali kadhalika, Data Na. 4(e na f) inaonesha sauti /s/ hutumika badala ya sauti /Ɵ/ katika maneno hayo. Mahusiano baina ya fonimu hizi ni kuwa zote ni vikwamizi. Hivyo basi, fonimu /s/

ya Kimaswamu imetumika badala ya fonimu ya Kiswahili /Θ/ ambayo haipo katika Kimaswamu katika harakati za ukopaji wa nomino. Mabadiliko ya fonimu hizi yanaukiliwa na nduni bainifu zinazohusiana kama ifuatavyo:

| /θ/ | → | /s/ |
|---|---|---|
| + konso | | +konso |
| + konti | ⇒ | +konti |
| - ghuna | | - ghuna |
| + ante | | +ante |
| - koro | | +koro |

Hapa tunaona sifa zote zinafanana kasoro sifa ya ukorona ndio inatofautiana katika sauti hizo.

Kubadika kwa sauti hizo kunaonekana kuchangiwa na mazingira maalumu ya mfanano wa kifonetiki. Pia, hali hiyo inadhihirisha kuwa, katika Kimaswamu, sauti /s/ inatumika badala ya sauti tatu zilizopo katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu Kimaswamu hakina sauti hizo katika msamiati wake. Hali hii inajitokeza pia katika lugha zingine ingawa kwa namna tofautitofauti. Kwa kufananisha, Ohly (1987) anaeleza pia kuwa matamshi ya sauti za Kiingereza na Kiswahili hutofautiana. Anatoa mfano wa sauti /ž/ katika istilahi *television* ya Kiingereza kwamba hubadilika na kuwa sauti /ʃ/ katika istilahi *televisheni* ya Kiswahili.

Mchakato wa kubadilisha sauti unatokea pia katika sauti /r/. Sauti /l/ hutumiwa badala ya /r/, kama inavyooneshwa katika Data Na. 5(a-c) katika nomino za Kimaswamu zilizotoholewa.

Data Na. 5

*a.* *Kilistoofa*
*Kilistoofa*
"Kristofa"

*b.* *ilidafutaali*
*i-li-dafutaali*
*kat-5-daftari*
"daftari"

*c.* *ilitileekita*
*i-li-tileekita*
*kat-5-tileekita*
"trekta"

Katika data hii, Data Na. 5(a-c) inaonesha namna sauti /l/ inavyotumika katika Kimaswamu badala ya sauti /r/ iliyopo katika lugha ya Kiswahili. Mahusiano baina ya fonimu hizi ni kuwa zote ni vilainishi ambavyo ni vya ufizi. Utokeaji huo unadhirishwa na mfanano wa sifa za kifonetiki zifuatazo:

$$
\begin{matrix} \textbf{/l/} & \longrightarrow & \textbf{/r/} \\
\left\{\begin{matrix} +\text{konso} \\ +\text{sono} \\ +\text{tamba} \\ +\text{ante} \end{matrix}\right\} & \Longrightarrow & \left\{\begin{matrix} +\text{konso} \\ +\text{sono} \\ -\text{tamba} \\ +\text{ante} \end{matrix}\right\}
\end{matrix}
$$

Hapa tunaona sifa zote zinafanana kasoro sifa ya utambaza ndio inatofautiana katika sauti hizo.

Hata hivyo, matumizi ya sauti /l/ badala ya sauti /r/ yanachochewa na mfanano wa sifa za kifonetiki, yaani sauti hizi zote hutamkiwa katika ufizi na wakati zinatamkwa kuna ulainishi fulani unajitokeza.

Kwa upande mwingine, mchakato wa kubadilisha sauti unatokea katika irabu. Sauti /i/ hutumika badala ya sauti /ɔ/, na sauti /ɔ/ hutumika badala ya sauti /i/ kama inavyooneshwa katika Data Na. 6(a-d) katika maneno ya Kimaswamu yaliyotoholewa.

Data Na. 6

*a.* *Pilaati*
“Pilato”

*b.* *Kiliisiti*
“Kristo”

*c.* *Setaano*
“Shetani”

*d.* *Zabuloono*
“Zabloni”

Data Na. 6(a na b) inaonesha kuwa mabadiliko haya ya irabu ni tofauti na yale ya konsonanti kwa sababu irabu hizi zote zipo ila zimebadilika katika baadhi ya nomino, hasa za majina ya pekee. Mabadililiko haya husababishwa na ukuruba fulani wa kifonetiki baina ya irabu hizi kutegemea mwinuko wa ulimi, irabu /i/ ni ya juu na irabu /ɔ/ ni ya kati juu. Utokeaji huo unadhirishwa na mfanano

wa sifa za kifonetiki zifuatazo:

| /ɔ/ | → | / i/ |
|---|---|---|
| + irabu<br>+kati<br>+ nyuma | ⇒ | +irabu<br>+ juu<br>+ mbele |

Irabu ya nyuma /ɔ/ hubadilika na kuwa irabu/ i/ ya mbele na kinyume chake. Vilevile, irabu hizi zina uhusiano unaotokana na ulalo wa ulimi; irabu / i/ ni ya mbele na irabu /ɔ/ ni ya nyuma. Mogaka (2012) anaeleza kuwa ukaribiano huo hufananafanana kifonetiki na anatoa mifano ya nomino za Kiswahili zilizotoholewa katika Kigusii kama vile ***kijiko***, ***vitunguu*** na ***pasi***. Maneno hayo yametoholewa katika Kigusii kama, *eγečiko*, *eβitunguo* na *eβasi*.

**Urefushaji**

Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa baadhi ya nomino zilizotoholewa kutoka lugha ya Kiswahili kwenda Kimaswamu hupitia mchakato wa urefushaji. Huu ni mchakato wa kifonolojia ambapo sauti fupi katika lugha changizi hurefushwa pindi inapotoholewa katika lugha pokezi. Mchakato huu unajidhihirisha katika Data Na. 7(a-c).

Data Na. 7

*a.* *itoochi*<br>*i- Ø-toochi*<br>*kat-9-tochi*<br>"tochi"

*b.* *ilijeneleeta*<br>*i-li-jeneleta*<br>*kat-5-jeneleeta*<br>"jenereta"

*c.* *ipiingu*<br>*i- Ø-piingu*<br>*kat-9-pingu*<br>"pingu"

Data Na. 7(a-c) inaonesha kuwa, katika Kimaswamu, irabu zimerefushwa wakati katika Kiswahili zilikuwa irabu fupi. Hivyo, baadhi ya nomino za Kiswahili zenye irabu fupi, zinapotoholewa katika Kimaswamu, hubadilishwa na kuwa irabu ndefu. Hata

hivyo, urefushaji huo hutokea katika mazingira ya kuwa katikati ya konsonanti. Kutokana na ruwaza ya data tuliyoitumia tunaunda kanuni ifuatayo:

$$/I/ \not\rightarrow [I:] \quad /K\text{-}K/$$

/+ Irabu / > [Irabu ndefu] / /+Kons _+Kons/

Kanuni hii inaonesha utokeaji wa irabu ndefu inapokuwa imetanguliwa na konsonanti halisi na kufuatiwa na konsonanti halisi. Hali hii hujitokeza pia katika baadhi ya lugha za Kibantu. Kwa mfano, Sote (2011) anaeleza kuwa irabu fupi katika maneno ya Kiswahili huwa ndefu pindi maneno hayo yanapotoholewa katika Kimalila hubadilishwa na kuwa irabu ndefu. Kwa mfano, maneno ya Kɨmalɨla *ichaaki*, *isiimu*, *ijeembe* na *impiingwa* yana irabu ndefu ilhali katika Kiswahili maneno hayo ni *chaki*, *simu*, *jembe* na *pingu* yakiwa na irabu fupifupi.

Aidha, urefushaji katika Kimaswamu unaashiria uasilishaji wa viarudhi katika maneno mkopo hayo. NZF inaeleza kuwa fonimu zinavyotumika katika lugha yoyote ile huweza kupangwa katika makundi asilia. Ili vitamkwa fulani viweze kuwa katika kundi asilia mojawapo, lazima viwe vinachangia sifa kadhaa za kimatamshi. Kwa hiyo, katika Kimaswamu urefushaji wa irabu hudhihirisha sifa za matamshi asilia zilizopo katika mfumo wa Kimaswamu ambapo hulazimisha irabu fupi za Kiswahili ziwe ndefu katika Kimaswamu. Kwa mujibu wa Morrison (2011), lahaja za Kibena zina toni. Toni hizo zina uamilifu wa kileksika na kisarufi katika msamiati wake. Pia, kuna madai ya baadhi ya wataalamu kama vile Kenstowizs na Suchato (2006) kuwa utohozi wa maneno mkopo huhusisha marekebisho yanayoongozwa na masharti ya lugha pokezi. Wanadai kwamba mzungumzaji huwa na nia ya kudumisha uaminifu kwa lugha changizi na wakati huohuo kufanya maneno mkopo kuwa na ruwaza ya vipandesauti na sifa arudhi ambazo zinakubalika katika lugha pokezi. Hivyo, katika nomino mkopo za Kimaswamu zinazotoholewa kutoka katika lugha ya Kiswahili, irabu nyingi zinazorefushwa huwa ni zile ambazo zina mkazo msingi. Hata hivyo, kipengele hiki kinaweza kuchunguzwa zaidi katika utafiti mwingine.

## Michakato ya Kimofolojia

Pamoja na kuangazia michakato ya kifonolojia, utafiti huu umeshughulikia pia michakato ya kimofolojia. Uchambuzi wa data katika michakato hiyo umeongozwa na NML. Nadharia hii iliongoza uambishaji wa viambishi awali vitangulizi na viambishi ngeli kwa sababu inaonesha mazingira mwafaka ambamo huruhusu nomino kuundwa kutokana na sheria zinazojidhihirisha kihatua. Katika vipengele vinavyofuata, michakato ya kimofolojia inayojitokeza katika nomino za Kimaswamu zilizotoholewa kutoka lugha ya Kiswahili inawasilishwa.

## Uambishaji

Utafiti huu umebaini kuwa nomino mkopo za Kimaswamu huwa na kiambishi awali kitangulizi, kiambishi ngeli na mzizi. Viambishi hivyo hupachikwa kabla ya mzizi kwa mchakato wa uambishaji. Aidha, nomino za Kiswahili ambazo kwa kawaida huwa na kiambishi ngeli na mzizi zinapotoholewa kwenda Kimaswamu, zinalazimika kufuata muundo wa nomino za lugha pokezi. Kwa kuanza, tutaonesha viambishi awali vitangulizi ambavyo huambikwa kabla ya kiambishi ngeli husika, kama Data Na. 8 (a-d) inavyoonesha katika nomino za Kimaswamu zilizotoholewa kutoka katika Kiswahili.

Data Na. 8

***a.*** ***i****simeenti*
***i****-simeenti*
"simenti"

***b.*** ***i****liita*
***i****-liita*
"lita"

***c.*** ***i****naamba*
***i****-naamba*
"namba"

***d.*** ***u****mwaaha*
***u****-mwaaka*
"mwaka"

Data Na. 8 (a-d) inaonesha namna uambikaji wa viambishi

kabla ya viambishi awali vitangulizi na kabla ya viambishi ngeli. Viambishi hivi huambikwa katika nomino mkopo zote isipokuwa majina ya pekee tu kama vile *Daviidi*, *Pilaati* na *Zabuloono.* Hoja hii pia inaungana na madai ya McCarthy (2002) anayeeleza kuwa mchakato wa kimofolojia unaotumika kwa wingi kwenye utohozi wa nomino za Kiswahili zinazoingia katika Kijaluo ni uambishaji. Hata hivyo, namna uambishaji huo unavyojitokeza hutegemeana na lugha mahususi. Aidha, wakati lugha nyingi za Kibantu zina nomino zenye viambishi awali vitangulizi, viambishi ngeli na mzizi, kama ilivyo katika Kimaswamu, nomino za Kiswahili zina kiambishi ngeli na mzizi pekee. Wataalamu mbalimbali kama vile Katamba (2003) Petzell (2008), Mbope (2016) na Goodness (2017) wanakubaliana kuwa kiambishi awali kitangulizi ni kipashio cha kimofolojia ambacho hutokea kabla ya kiambishi ngeli cha nomino. Mathalani, zipo lugha zenye maumbo sahili na maumbo changamani ya viambishi awali vitangulizi huku zikitofautiana katika idadi ya maumbo hayo. Kwa mfano, maumbo sahili ya irabu (I) ni kama vile: *{o, a,* na *e}* katika Kizulu S42 (De Blois, 1970) na Kiganda E15 (Katamba, 2003). Kwa upande mwingine, maumbo changamani ya Konsonanti-Irabu (KI) hutokea katika baaadhi ya nomino za lugha kama vile Kiluguru G15 (Mkude, 1974). Aidha, maumbo changamani ya Irabu-Konsonanti-Irabu (IKI) hutokea katika lugha kama vile Kizigua G32 (De-Blois, 1970).

Vilevile, nomino za Kimaswamu zilizokopwa kutoka Kiswahili hufuata utaratibu wa lugha ya Kimaswamu na kuwekwa katika ngeli za kimofolojia za Kimaswamu. Mfumo wa ngeli ni tabia ya kimuundo iliyopo katika lugha za Kibantu unaohusu nomino (Maho, 1999). Kutokana na tabia hii, wataalamu mbalimbali wameweza kugawanya nomino za lugha mbalimbali za Kibantu katika makundi mbalimbali yanayojulikana kitaalamu kama ngeli, kwa msingi wa aina ya viambishi awali ambavyo huambikwa kwenye mizizi hiyo.

Ili kurasmisha utaratibu huo, makundi ya nomino (ngeli) yalipewa namba. Kigezo cha kuzingatia namba kiliasisiwa na Bleek (1869) ambaye alibainisha takribani makundi 22 ya ngeli miongoni mwa

lugha za Kibantu katika eneo la Kusini mwa Afrika (Mkuria, 2002). Utaratibu huo umewezesha kujua idadi ya ngeli za nomino katika lugha za Kibantu. Hivyo, utaratibu wa kupanga ngeli katika namba umetumika katika kuainisha ngeli za nomino za Kimaswamu. Mutaka na Tamanji (2000) wanaeleza mifumo ya nomino katika lugha za Kibantu kuwa inaweza kubainishwa kwa namna tatu kama ifuatavyo:

a. ka+sh
b. kat+ka+sh
c. kaf+ka+sh

**Ufunguo:**

| | | |
|---|---|---|
| Ka | = | kiambishi awali |
| Kat | = | kiambishi awali tangulizi |
| Kaf | = | kiambishi awali fuatizi |
| Sh | = | Shina |

Mifumo hii, ambayo ni ya jumla kwa ajili ya lugha za Kibantu, si lazima ijitokeze yote katika kila lugha. Kwa mfano, katika Kimaswamu mfumo (b) kat + ka+ sh ndio unaojitokeza zaidi katika nomino. Kimaswamu hakina mfumo (a) ka+ sh, na (c) kaf + ka + sh. Hata hivyo, Kimaswamu kina mfumo mwingine katika baadhi ya nomino ambao haukuainishwa na Mutaka na wenzake (2000), ambao ni kat + kaf + ka + sh. Kwa hiyo, Kimaswamu kina mifumo miwili ya nomino ambayo ni katAT+ka+sh na kat+kaf+ka+sh. Ijapokuwa mfumo wa nomino wa Kimaswamu una kiambishi awali tangulizi (kat) na kiambishi awali fuatizi (kaf), uainishaji wa nomino katika ngeli unafanywa kwa misingi ya viambishi awali vinavyoashiria umoja na wingi kama ilivyofanyika kwenye lugha zingine za Kibantu, kama Data Na. 9 (a- b) inavyoonesha.

Data Na. 9

(a) *u+muu+nu* "mtu", *a+vaa+nu* "watu"
*kat 1 Sh* *kat 2 Sh*

(b) *i+ li+muu+nu.* "jitu", *a+ma+muu+nu* "majitu"
*kat kaf1 Sh* *kat kaf1 Sh*

Data Na. 9 inaonesha kwamba viambishi ngeli hutokea mwanzoni, hufutia kaimbishi awali fuatishi na mwisho shina la neno.

Kutokana na uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka kwa watoataarifa uwandani, nomino zote zilizotoholewa zinazohusu watu huingizwa katika ngeli ya 1/2, kama Data Na. 10 (a na d) inavyoonesha.

Data Na. 10

| | | |
|---|---|---|
| *a.* | ***umu**kiliisiti* | ***ava**kiliisiti* |
| | *u-**mu**-kiliisiti* | *a-**va**-kiliisiti* |
| | *kat-1-kiliisiti* | *kat-2-kiliisiti* |
| | "Mkiristo" | "Wakristo" |
| *b.* | ***umu**dakitaali* | ***ava**dakitaali* |
| | *u-**mu**-dakitaali* | *a-**va**-dakitaali* |
| | *kat-1-dakitaali* | *kat-2-dakitaali* |
| | "daktari" | "madaktari" |
| *c.* | ***umu**suungu* | ***ava**suungu* |
| | *u-**mu**-suungu* | *a-**va**-suungu* |
| | *kat-1-suungu* | *kat-2-suungu* |
| | "mzungu" | "wazungu" |
| *d.* | ***umu**jelumaani* | ***ava**jelumaani* |
| | *u-**mu**-jelumaani* | *a-**va**-jelumaani* |
| | *kat-1-jelumaani* | *kat-2-jelumaani* |
| | "Mjerumani" | "Wajerumani" |

Data Na. 10 inaonesha kuwa, katika maneno mkopo ya ngeli ya 1, kiambishi {-mu-} na ya ngeli ya 2, kiambishi {-va-} hupachikwa kabla ya shina la neno.

Aidha, kwa mujibu wa data za utafiti huu, zipo nomino zingine ambazo zimetoholewa na huwekwa katika aina zingine za ngeli, kama vile ngeli ya 3/4, 5/6, 7/8 au 9/10 kama Data Na. 11(a-e) inavyoonesha.

Data Na. 11


| | | |
|---|---|---|
| *a.* | ***umu**tuuka* | ***imi**tuuka* |
| | *u-**mu**-tuuka* | *i-**mi**-tuuka* |
| | *kat-3-tuuka* | *kat-4-tuuka* |
| | "motokaa" | "motokaa" |
| *b.* | *iliduuka* | *amaduuka* |
| | *i-**li**-duuka* | *a-**ma**-duuka* |
| | *kat-5-duuka* | *kat-6-duuka* |
| | *"duka"* | *"maduka"* |

| | |
|---|---|
| c. ***ii*** *taabu* | ***ifi*** *taabu* |
| *i-**i**-taabu* | *i-**fi**-taabu* |
| *kat-7-taabu* | *kat-8-taabu* |
| *"kitabu"* | *"kitabu"* |
| d. *inyumba* | *inyumba* |
| *i-N-yumba* | *i-N-yumba* |
| *kat-9-yumba* | *kat-10-yumba* |
| *"nyumba"* | *"nyumba"* |
| e. *imeeza* | *imeeza* |
| *i- Ø-meza* | *i- Ø-meza* |
| *k.a.t.-9-meza* | *k.a.t.-10-meza* |
| *"meza"* | *"meza"* |
| f. *irediio* | *irediio* |
| *i- Ø-rediio* | *i- Ø-rediio* |
| *k.a.t.-9-redio* | *k.a.t.-10-redio* |
| *"redio"* | *"redio"* |

Data Na. 11 inaonesha kuwa maneno mkopo hupachikwa viambishi ngeli katika ngeli husika ili kuendana na mfumo wa lugha ya Kimaswamu. Katika ngeli ya 3, kiambishi {mu} huchopekwa; katika ngeli ya 4, kiambishi {mi} huchopekwa; na katika ngeli ya 5, kiambishi {li} huchopekwa. Aidha, katika ngeli ya sita 6, kiambishi {ma} huchopekwa; katika ngeli ya 7, kiambishi {i} huchopekwa; na katika ngeli ya 8, kiambishi {fi} huchopekwa. Kadhalika, katika ngeli ya 9/10, mara nyingi hakuna kiambishi dhahiri. Hata hivyo, maneno mkopo mengi huwekwa ngeli ya 9/10. Upangaji wa nomino katika ngeli hujitokeza pia katika lugha nyingine. Kwa mfano, Stephano (2023) anaeleza kuwa nomino za Kiswahili zinazokopwa na kupokelewa katika Gɪrɪmi huwekwa katika ngeli za MU-/WA-; MU-/MI-; JI-, Ø-/MA-; KI-/VI-; N-/N-; U-/N-;U-/MA-; na KU-, ambapo maumbo ya umoja na wingi, pamoja na sauti, huchakatwa kulingana na mfumo lugha wa Gɪrɪmi. Hata hivyo, utokeaji wake hutofautiana miongoni mwa lugha kadhaa. Kwa mfano, Okombo (1982) anaeleza kuwa mofimu za wingi katika nomino za Kijaluo huwakilishwa na viambishi tamati {-i}, {-e} au {-ni} na hutokea baada ya mzizi wa neno.

Baada ya kuelezea michakato hiyo, tumeziweka kwa muhtasari hatua za upachikaji wa kiambishi awali kitangulizi na kiambishi ngeli kwa kutumia Kielelezo Na. 2 kama mchakato unavyojidhihirisha kupitia NML.

**Kielelezo Na. 2: Namna Michakato ya Kimofolojia Ilivyofanyika**




Kielelezo Na. 2 kinaonesha kwamba michakao ya kimofolojia hufanyika kihatua. Kwanza, kunakuwa na umbo mzizi (leksikoni). Baada ya hapo, kuna kupachika kiambishi awali tangulizi {u}. Halafu inafuata hatua ya kupachika kiambishi {*mu*} katika mazingira ya [$Ng_5$_____ $SN_5$] (nomino umoja); ambapo $Ng_5$ = kiambishi cha ngeli ya tano, na $SN_5$ = shina la nomino ya ngeli ya tano. Baada ya hapo, neno hilo linajidhihirisha kimatamshi katika Kimaswamu. Mwisho, neno hilo linaweza kutumika katika miktadha mbalimbali ya kisintaksia.

## Hitimisho

Lugha mbalimbali huwa na nomino mkopo. Mchakato wa kuasilisha nomino hizo huweza kutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Suala hili lilichochea kufanyika kwa utafiti uliozaa makala hii katika Kimaswamu. Imebainika kuwa ipo michakato ya kifonolojia na kimofolojia ambayo hujitokeza wakati wa kuasilisha nomino mkopo kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kimaswamu. Michakato ya kifonolojia iliyobainika ni uchopezi, udondoshaji, ubadilishaji sauti na urefushaji irabu. Michakato hiyo hutokana na mazingira kadhaa yaliyojitokeza katika fonimu. Mchakato wa kimofolojia uliotawala ni wa uambatizi ambapo viambishi awali vitangulizi na viambishi ngeli hupachikwa katika nomino mkopo zinazohusika ili kuendana na muundo wa Kimaswamu. Utafiti huu ulijielekeza katika vipande sauti. Hata hivyo, viarudhi kama toni na mkazo viligusiwa tu katika urefushaji wa irabu. Kwa kuwa utafiti huu ulishughulikia michakato inayohusu vipandesauti, inapendekezwa kuwa uchunguzi mwingine ufanyike katika utohozi wa viarudhi katika maneno ya Kimaswamu yaliyotoholewa kutoka Kiswahili ili kubaini uwakilishi wa viarudhi unavyojitokeza katika maneno hayo. Pia, utafiti ufanyike katika aina nyingine za maneno yaliyotoholewa kama vile vitenzi ili kubaini michakato ya utohozi inavyojitokeza na athari zake.

## Declaration of conflicting interests

The author(s) declared no conflict of interest(s) with respect to the research, authorship and/or publication of this paper.

## Funding

The author(s) declared that the research was privately funded.

## Marejeleo

Adicka, O. P. (2016). *Utohozi wa Maneno-mkopo katika Lugha ya Kijaluo kutoka Kiswahili: Mtazamo wa Mlingano Chanzi.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Adolph, E. (2014). *Utohozi wa Nomino za Kiswahili na Athari yake katika Ngeli za Kihaya.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Aswani, F. O. B. (2001). *Uswahilishaji Kifonolojia wa Maneno yenye Asili ya Kiingereza Katika Kiswahili Sanifu.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton.

Bleek, W. H. I. (1869). *A Comparative Grammar of South African Languages: Part 2.* London: Truber & Co.

Chaula, E. H. Y. (1989). *Aspects of Ki-Bena Phonology: The Case of Kimavemba Variety.* Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

Chaula, E. H. Y. (2017). Properties of Word Categories in Kibena: Nouns, Verbs and Adjectives. Unpublished PhD Thesis, University of Dar es Salaam.

Chomsky, N. & Halle, M. (1968). *The Sound pattern of English.* New York: Harper & Row.

Crystal, D. (2008). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics (*6th Edn.). UK: Blackwell Publishing Ltd.

Dawson, C. (2002). *Practical Research Methods.* Magdalen Road Ox4 1RE United Kingdom: Oxford University Press.

De Blois, K. F. (1970). The Augment in the Bantu Languages. *Africana Linguistics*, 4: 85–165. https://www.persee.fr/doc/aflin_2033-8732_1970_num_4_1_879

Goodness, D. (2017). The Bantu Preprefix, Morphology, Phonology or Syntax. *International Journal of Linguistics*, 9: 1–14. https://doi.org/10.5296/ijl.v9i3.1133

Haspelmath, M. & Tadmor, U. (2009). *Loanwords in the World's Languages Comparative Handbook.* Berlin: Mouton de Gruyter.

Haugen, E. (1950). The Analysis of Linguistic Borrowing. *Language,* 26: 210–231. https://doi.org/10.2307/410058

Hickey, R. (2010). *The Handbook of Language Contact.* Malden U.S.A: Blackwell and Publishing Ltd.

Iribemwangi, P. I. & Mukhwana, A. (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus Publishers.

Iribemwangi, P. I. (2013). Cultural Transfer from Europe and Asia to Africa: Evidence from Borrowed Lexicon Adapted into Kiswahili. *International Journal of Education and Research*, 1(8): 1–14.

Jensen, J.T. (2004). *Principles of Generative Phonology: An Introduction.* Amsterdam: John Benjamins Publishing House.

Kahigi, K. K. (2007). Ujanibishaji wa Office na Windows XP kwa Kiswahili Sanifu.*Kioo cha Lugha*, 5: 70–99. https://doi.org/10.4314/kcl.v5il.61504

Kang, Y. (2003). Perceptual Similarity in Loanword Adaptation: English Postvocalic Word-Final Stops in Korean. *Phonology*, 20(02), 219–273. https//doi:10.1017/s0952675703004524.

Karuru, I. (2012). *Pholonogical and Morphological Adaptation of Gi – Gichugu: An Application of Source – Similarity Model.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Katamba, F. (2003). Bantu Nominal Mophology. In D. Nurse & G. Phillippson (eds.). *The Bantu Languages.* London: Routledge.

Kayigema, J. & Mutasa, D. (2015). Peculiarities of Loanwords in Kinyarwanda Noun Class. *Journal of Educational Research and Studies*, 3(3): 57–65. https://silo.tips/www.peakjournals.org

Kiparsky, P. (1982b). From Cyclic Phonology. In H. Ver Der & N. Smith (eds.). *The Structure of Phonology Representation.* U.S.A: Foris Publication.

Kothari, R. C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques* (2nd Ed.). New Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

LaCharité, D. & Paradis, C. (2005). Category Preservation and Proximity versus Phonetic Approximation in Loanword Adaptation. *Linguistic Inquiry*, 36: 223–258.

Lodhi, A. (2000). *Oliental Influences in Swahili: A Study in Language and Culture Contacts.* Goteborg Acta: University of Gothoburgensis.

Lusekelo, A. (2018). Lexical Borrowing in Africa with Special Attention to Outcomes of Languages in Contacts in Tanzania. *Journal of African Studies*, 7.2: 1–22. https://www.ajol.info/index.php/mjas/article/view/173171

Maho, J. (1999). *A Comparative Study of Bantu Noun Classes.* Unpublished PhD Dissertation, Goteborg Universty.

Maho, J. F. (2009). A Referential Classification of the Bantu Languages. Retrieved from goto.glocalnet.net/mahopapers/nuglonline.pdf, on 16/3/2023.

Masele, B. F. Y. P. (2001). *The Linguistic History of Sisuumbwa, Kisukuma and Kinyamwezi in Bantu Zone F.* Unpublished PhD Thesis, Memorial University of Newfoundland.

Massamba, D. P. B (2011). *Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia.* Dar es Salaam: TUKI.

Matiki, A. J. (2016). Patterns of Lexical Borrowing in Chichewa. *Journal of Linguistics Association of Southern African Development Community Universities*, 4(4): 79–93. https://journals.ub.bw/index.php/lasu/article/view/671

Mbope, N. (2016). *A Study of Nominal Pre-prefix in Kinyakyusa.* Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar es Salaam.

McCarthy, A. C. (2002). *An Introduction to English Morphology: Words and their Structure.* Edinburg: Edinburg University Press.

Mkude, D. (1974). *A Study of Kiluguru Syntax with Specal Reference to the Transformational History of Sentences with Permuted Subject and Object.* London: London University Press.

Mkuria, D. M. (2002). Tathmini ya Vigezo Vinavyotumiwa Kufundishia Ngeli za Kiswahili. *Utafiti wa Kiswahili*, 1: 141–148.

Morrison, M. E. (2011). *A Reference Grammar of Bena.* Unpublished PhD Thesis, University of Rice.

Mosota, K. E. (2016). *Utohozi wa Msamiati kutoka Kiswahili hadi Ekegusii.* Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi.

Msuya, J. & Mreta, A. Y. (2019). Adaptation of Loanwords in Chasu. *Journal of Linguistics and Language in Education*, 13(1): 26–46.

Mutaka, N. & Tamanji, P. N. (2000). *Introduction to African Linguistics.* Muenchen: Lincom Handbooks in Linguistics.

Mwendamseke, F. (2011). *Uainishaji wa Ngeli za Nomino katika Kibena.* Tasinifu yaUmahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Nassor, F. (2017). *Kuchunguza Sababu za Upungufu wa Istilahi za Kiswahili za Kufundishia Sayansi na Teknolojia katika Shule za Msingi: Mfano wa Kisiwa cha Pemba.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Njogu, K., Mwihaki, A. & Buliba A. (2006). *Sarufi ya Kiswahili Uchanganuzi na Matumizi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Ohly, R. (1987). *Primary Technical Dictionary* (*English–Swahili*). Dar es Salaam: IPI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Okombo, D. (1982). *Dholuo Morphophonemics in a Generative Framework.* Berline: Beiner.

Ola H. (2022). Phonological and Morphological Integration of Loanwords into Egyptian Arabic. *Égypte/Monde arabe*, 27–28: 1–24. https://doi.org/10.4000/ema.1958

Peperkamp, S. & Dupoux, E. (2001). *Loanwords Adaptations: Three Problems for Phonology and Psycholinguistic Solution. Laboratoire de Sciences Cognitive et Psycholinguistique.* Paris: Universite de Paris.

Petzell, M. (2008). *The Kagulu Language of Tanzania: Grammar, Text and Vocabulary.* Cologne: Rüdiger Köppe Verlag.

Rubach, J. (1984). *Syclic and Lexical Phonology: The Structure of Polish*. USA: Foris Publications.

Rwamo, A. & Ntiranyibagira, C. (2020). Phonological and Perceptual Factor Symbiosis in Loanword Adaptation: A Case Study of Kirundi. *Revista Odisseia*, 5(1): 22–39.

Sote, A. (2011). *Nativization Process of Kiswahili Borrowed Nouns into Shimalila*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Stephano, R. (2023). Mapokezi ya Nomino za Kiswahili katika Ngeli za Nomino za Girimi. *Utafiti*, 18: 225–242. http://doi.org/10.1163/26836408-15020085

Ström, E. & Miestamo, M. (2020). The Use of Augment ni Nguni Languages with Special Refference to Referentiality of the Noun, In L. Marten, R. Ǵuerois, H. Gibson & E. Ström (eds.). *Morphosintactic Variation in Bantu*. Oxford: Chuo Kikuu cha Oxford, 114-128.

Zibin, A. (2019). A Phonological Analysis of English Loanwords Inflected with Arabic Morphemes in Urban Jordanian Spoken Arabic. *SAGE Open*, 9(2): 1–13. https://doi.org/10.1177/2158244019841927.

**Kiambatisho 1: Alama za Unukuzi Zilizotumika na Maana Zake**

| Alama | Maana |
|---|---|
| I | Irabu |
| K | Konsonanti |
| KI | Konsonanti na Irabu |
| [ ] | Unukuzi wa kifonetiki |
| / / | Uwasilishaji wa fonimu |
| { } | Uwakilishi wa mofu |
| > / | Badiliko kutoka Kiswahili kuelekea Kimaswamu |
| # | Mpaka wa neno |
| / | Katika mazingira ya |
| Ш | Mofu kapa |
| + | Kuwepo na sifa fulani |
| - | Kutokuwepo na sifa fulani |

## Author Biography

Faraja Mwendamseke is a lecturer in Linguistics (Kiswahili Unit) in the Department of Languages and Literature at the Dar es Salaam University College of Education, University of Dar es Salaam. Her research interests are in Phonology, Morphology and Second language learning. Her recent publications are Uchanganuzi wa Mkazo katika Maneno ya Kiswahili Sanifu (Mwanga wa Lugha, 2023) and Ufaafu wa Matumizi ya Nadharia ya Utabia katika Mbinu za Kufundishia Lugha ya Kigeni (Kioo cha Lugha, 2022; with S. Bichwa).